# Shamba la mifugo Ngerengere labadilisha maisha ya wananchi Morogoro

NA MWANDISHI WETU



KWA kutambua mchango wa Sekta ya Mifugo, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi diamua kuwekeza katika mashamba ili kuyapa uwezo wa kuzalisha mifugo bora itakayowasaidia kukuza kipato cha familia na wananchi kwa ujumla.

Ngerengere ni miongoni mwa mashamba makubwa ya Serikali yaliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kata ya Ngerengere mkoani Morogoro.

**Historia ya Shamba la LMU Ngerengere**

Meneja wa Shamba la Serikali (LMU) Ngerengere, Saita Ole Kimosa anasema shamba hilo lilianzishwa mwaka 1975 kama shamba la ng'ombe wa maziwa ambalo katika lilifahamika kama Dairy Farm Company lililokuwa chini ya wakati huo baadaye likifikia na kubadilishwa jina na kuitwa LMU mnamo mwaka 2004 chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Meneja huyo anaendelea kueleza lengo la kuanzishwa kwa shamba hilo kuwa ni pamoja na kuzalisha mifugo bora yenye tija na kuuziwa wananchi kwa bei ambayo ni rafiki na kujiongezea kipato na kusaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.

Saita anasema hadi Mei 2020 shamba lilikuwa na mifugo mbalimbali ikiwemo ng'ombe 771 mbuzi 234, na nguruwe 201 na limekuwa na uzalishaji mzuri, pia ameeleza aina ya mifugo iliyopo kuwa ni ng'ombe aina ya borani, fresian na chotara, kwa upande wa mbuzi alitaja aina ya boa ambayo asili yake ni Afrika ya Kusini na nguruwe aina ya landress na large white.

**Mafanikio ya shamba tangu kuanzishwa kwake**

Akizungumzia mafanikio ya shamba hilo ambalo lina mifugo takribani 1,206 (elfu moja mia mbili na sita) Meneja huyo anasema shamba hilo limefanikiwa kuzalisha mifugo mingi na kuisambaza kwa kuwauzia wafugaji wadogo wadogo kwa bei ambayo ni rafiki katika mkoa wa Morogoro na Dar es Salaam.

Meneja Kimosa anaeleza shambani hapo kuna mifugo ya aina tatu ikiwa ni ng'ombe mbuzi na nguruwe ambayo yote inauzwa kwa wananchi kwa bei rafiki ili kusaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.

Anaendelea kufafanua kila aina ya mifugo iliyopo shambani hapo kwa kusema, wana ng'ombe aina ya borani, freshian na chotara na kusema kuwa chotara wanapatikana kwa kupandisha borani na freshian na kuongeza kuwa chotara wanaopatikana hapo wana sifa ya kutoa maziwa mengi.

Aidha kuna mbuzi aina ya boa asili yake ikiwa ni Afrika ya Kusini na ni mbuzi wa nyama na wanatumika kama mbegu kwa wafugaji na wanaweza kupandishwa na mbuzi wa kienyeji na kupata chotara wazuri na wanaokua haraka sana. Pia kuna nguruwe aina ya largewhite na landres ambao wanatumika kwa lengo la kuuzwa kwa wananchi kwa ajili ya mbegu bora.

**Mchango wa shamba la LMU Ngerengere kwa jamii inayowazunguka**

Kwa upande wa mchango Saita anasema wameweza kuwapatia wafugaji mitamba bora kwa bei nafuu baadhi ya wananchi kupata ajira ndani ya shamba la hilo la serikali, kuwauzia maziwa wananchi wanaozunguka shamba hilo pamoja na kuwapa makazi kwa ajili ya kulima.

Pia wafugaji wananufaika kwa kupata tiba ya mifugo na ushauri kutoka kwa wataalam wa shamba la mifugo la Serikali Ngerengere, wanahamasishwa kutenga mifugo yao na kufanya uhimilishaji kwa mifugo hiyo pamoja na kuuziwa madume bora ili kuboresha ng'ombe wa asili na kuwauzia chotara.

Hata hivyo meneja Saita anasema kipindi cha kiangazi kuna lambo linafahamika kama Mkobora limetengwa kwa ajili ya wananchi kunywesha mifugo yao ili kusaidia ng'ombe na mifugo mingine isife kwa kukosa maji maeneo hayo.

**Changamoto zinazokabili shamba hilo**

Hata hivyo Saita anaainisha changamoto ambazo zinakabili shamba hilo ikiwemo miundombinu mibovu pamoja uchakavu wa vitendea kazi ambayo hupelekea kushindwa kutimiza baadhi ya majukumu ya kila siku na kutoka eneo moja kwenda lingine kutoka na ubovu au kutokuwepo kabisa kwa usafiri.

Saita anaongezea kuwa, kipindi cha dotia wananchi hukasirishwa na wakati mwingine kuamua kuchoma moto baadhi ya maeneo ya shamba hili, pia kuna uvamizi mifugo sana wa wafugaji kuingiza mifugo na kulisha ndani ya shamba na kutoka.

**Mikakati katika kujikwamua.**

Kwa upande wa mikakati Saita anasema kuwa wanatarajia kila mwaka kufanya uzalishaji mkubwa wa mifugo wanze na kupata hela kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ya shamba na kutatua changamoto zilizo ndani ya uwezo wao.

Wito kwa wadau wa mifugo Ngerengere na nchi nzima kwa ujumla

Wito wa Saita kwa wadau wa mifugo ngerengere na nchi nzima ni kwamba mifugo ni rasilimali inayotoa ajira na ni malighafi ya viwanda, hivyo wananchi watumie malighafi hizo vizuri.

Aidha anawashauri wafugaji kutibu mifugo yao kwa wakati ili kuepusha magonjwa yasiyo ya lazima kwa wanyama na kuogesha angalau mara moja kwa wiki pamoja na kuchanja kwa wakati.

Anaendelea kuwashauri wafugaji kufuga kisasa na kwa tija kwani mifugo ndio ajira yenyewe, kuchagua mifugo iliyo bora kutunza na kutunza pia ngozi kwani kila kilichopo kwa ng'ombe ni mali pamoja na kuhimilisha mifugo yao ili kupata koo tofauti na kuepuka kudumaza mifugo kwa kuwa na koo moja inayozunguka kwenye boma, hii husaidia kupata mifugo bora na mizuri zaidi.

Kifuto Kimanga ni mkazi na mfugaji wa Kiwege, amesema kwa muda mrefu amekuwa akifanya ufugaji wa kuhamahama ambao ulisababisha yeye na familia yake kutokuwa na makazi maalumu maana kila siku wapo barabarani kutafuta maeneo ya kulisha mifugo yake na wakati mwingine kuingia kwenye migogoro na watumiaji wengine wa ardhi kutokana na mifugo kufanya uharibifu.

Anaendelea kusema kuwa ameamua kuachana na adha ya kuhama hama na kuamua kutafuta eneo la kudumu kwa ajili ya makazi na kufanya ufugaji wa kisasa ambapo shamba la LMU Ngerengere limemsaidia kupata mbegu bora za mifugo na za kisasa.

> Kipengele muhimu kabisa katika ndoa ni urafiki. Penye urafiki hakuna kizuizi kitakachoshindikana.

# SHAMBA LA MIFUGO NGERENGERE LAWA CHACHU YA UFUGAJI BORA MOROGORO

Inatoka Uk. 15

ama nyingi na maziwa mengi," Anasisitiza Kifuto.

Pia anasema kutokana na uwepo wa shamba hilo wanapata msaada wa kitabibu kwa mifugo yao kutoka kwa wataalam wa mifugo waliopo shambani hapo na elimu pia ya utunzaji bora wa mifugo yao.

Aidha anaelezea mafanikio aliyopata kutokana na ufugaji bora na wa kisasa kwani mwaka 2013 aliweza kujenga nyumba kubwa ya kisasa yenye uwezo wa kutatua watu 24 inayokidhi haja zao na kuweza kupeleka watoto shule nzuri na za kisasa.

Hata hivyo anaendelea kufafanua na mifugo hiyo kwani ameweza kuzalisha mbuzi kwa wingi na kuwauza kwa bei inayompa faida ambapo hapo awali alinunua mbuzi kwenye shamba la LMU Ngerengere kwa bei nafuu sana kwa dume moja alinunua 150,000 (laki moja na elfu hamsini) na kwa sasa yeye anauza kuanzia 250,000–300,000 (laki mbili na elfu hamsini hadi laki tatu) kwa



*Meneja wa Shamba la Mifugo la Serikali Ngerengere Saita Ole Kimosa akiongelea jinsi shamba hilo linavyowanufaisha wafugaji wa mkoa wa Morogoro na mikoa jirani.*

mbuzi mmoja ambapo anapata faida kubwa na ya kutosha kwa kuendesha maisha yake ya kila siku na kufanya maendeleo.

Kifuto anaendelea kusema kuwa mbuzi hao ni wakubwa sana, wanakuwa kwa haraka na wana nyama nyingi sana pia hawana tofauti na mbuzi wa Tanzania/asili zaidi sana ni kuzingatia matunzo, chanjo, dawa za minyoo na chakula cha kutosha chenye virutubisho vyote kwa mifugo.

Kwa upande wa ng'ombe anaelezea namna wanavyotoa maziwa kwa wingi kwa kutoa lita 14 kwa siku kila mmoja, nyama nyingi pindi wanapochinjwa na kuongezea kuwa wanawapa matunzo mazuri kwa kuzingatia kuwachanja kwa wakati, na kutoa huduma zote za matibabu kwa wakati ili kuepuka kupoteza ng'ombe kwa magonjwa yasiyo ya lazima.

Pia Esther Kilinga mfugaji wa Kwege jirani na shamba la LMU Ngerengere anaelezea namna alivyonufaika na shamba la LMU Ngerengere kwani ameweza kupata madume kutoka shambani hapo na kwa sasa ana punda ya ng'ombe 200 (mia mbili) na kutokana na mifugo hiyo amefanikiwa kujenga nyumba ya kisasa ya kuishi, nyumba za wageni (gesti) zinazowaingizia kipato na kuweza kuendesha maisha yao ya kila siku, wamejenga kanisa na kuwasomesha watoto kwenye shule nzuri na za kisasa.

Hata hivyo anauza maziwa, samli na mifugo hiyo hai kwa wanakijiji wa Ngerengere na maeneo jirani na hii hupelekea kunufaika na ufugaji wao na kuweza kuchangia pato la Taifa.

Aidha mfugaji mdogo na mkazi wa Ngerengere, Athumani Ramadhani anasema alianza ufugaji mwaka 2018 akiwa na ng'ombe watatu (3) na kufika sasa amefikisha ng'ombe kumi (10) na kuanzia faida alizozipata kutokana na ng'ombe hao ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba ya kisasa, ameweza kukidhi mahitaji ya familia yake ambapo hapo hawali hali ilikuwa mbaya.

Athumani anashukuru uwepo wa shamba la LMU Ngerengere kwani limeweza kuwasaidia wafugaji wengi kupata mbegu bora za mifugo inayowasaidia kuzalisha kwa wingi na kufundishwa kanuni za ufugaji bora na tiba kwa mifugo yao na kuweza kupata lita nane za maziwa kwa ng'ombe mmoja kwa siku. Hata hivyo anaiomba Serikali kusaidia kuwajengea josho wafugaji wa majumbuni kwani kwa kutumia solo kwa ng'ombe wengi ni kazi ngumu kwani pia dawa haiwafikii vizuri na wakati mwingine mifugo mingine hukwepa dawa hivyo kutofanikisha lengo la kuogesha.

Aidha anawashauri wafugaji wengine kutumia vizuri shamba la LMU Ngerengere kwani lipo kwa ajili yao na watapata mifugo bora na mizuri sana inayotoa maziwa lita nane kwa siku na kuongezea kuwa ng'ombe ni mali.

Anaendelea kwa kusema kuwa anawashauri wafugaji wenzake kufuga mifugo michache na yenye tija kuliko kufundika mifugo mingi ambayo haipati huduma nzuri na chakula na pia kutafuta maeneo ya kufugia na kuacha ufugaji wa kuhamahama kwani pia uharibu mazingira na kusababisha migogoro kati yao na watumiaji wengine wa ardhi.



*Ester Kilinga mmojawapo ya wafugaji walionufaika na shughuli za ufugaji kwenye kijiji cha Kwege ngerengere akiwa na familia yake.*



*Kifuto Kimanga, mfugaji wa kijiji cha Kwege, Ngerengere mkoani Morogoro akiwa mbele ya nyumba yake ya zamani kabla ya kuwa na makazi bora yaliyotokana na faida za mifugo hususani ng'ombe wanaopatikana kwenye shamba la mifugo la serikali Ngerengere.*



*Nyumba ya Mfugaji Bw. Kifuto Kimanga aliyoijenga baada ya kunufaika na ufugaji katika kijiji cha Kwege, Ngerengere mkoani Morogoro.*

Scanned with CamScanner

**Melo wa Jamii Forum ahukumiwa kifungo**



## Ofisa LATRA asimamishwa kazi kwa matumizi ya nguvu kazini

OFISA Leseni wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhi (LATRA), Mkoa wa Lindi, Emmanuel Manase, amesimamishwa kazi kwa tuhuma za matumizi ya nguvu yaliyopitiliza wakati wa kutekeleza majukumu...

# UHURU

ISSN 0876 - 3490 No. 23853 Jumatano Novemba 18, 2020 Tanzania sh 1,000
Ukweli Daima

WCF
Pata Huduma Mtandaoni
portal.wcf.go.tz
www.wcf.go.tz

# Meli 8 za uvuvi zitakavyopaisha uchumi wa nchi



KAPTENI GILBERT MOKIWA.

- **Samaki** wa mamilioni sasa wataweza kuvunwa na kusafirishwa kwenye soko la kimataifa na kuiingizia nchi fedha za kigeni
- **Meli** hizo zitatoa ulinzi wa maeneo ya bahari kuu dhidi ya walowezi waliokuwa wakivua eneo la Tanzania na kujinufaisha binafsi.





WAVUVI wakiwasili katika Soko la Samaki la Kimataifa Feri, Dar es Salaam. Picha ndogo kushoto mvuvi Faisal Ally akionyesha samaki aina ya sangara.

## Neema ya soko yaja kwa wakulima wa mahindi

- **Jitihada** za serikali zafanikisha kupatikana soko la uhakika Misri
- **Kampuni** nchini humo yaangalia uwezekano kwa mazao mengine

## Wanawake wajawazito wadaiwa kukwepa kuhudhuria kliniki